035713655

KENYA NATIONAL PREDICTION TESTS

# KCPE

516004

## KISWAHILI
## SEHEMU YA KWANZA
## LUGHA

**Muda: Saa 1 dakika 40**

**MAAGIZO KWA WATAHINIWA**
**SOMA MAAGIZO YAFUATAYO KWA MAKINI.**

1. Umepewa kijitabu hiki cha maswali na karatasi ya kujibia. Kijitabu hiki kina maswali 50.
2. Ukisha chagua jibu lako lionyeshe katika **KARATASI YA MAJIBU** na wala siyo katika kijitabu hiki cha maswali.

**JINSI YA KUTUMIA KARATASI YA MAJIBU**

3. Tumia penseli ya kawaida.
4. Hakikisha ya kwamba yafuatayo yameandikwa katika karatasi ya majibu:

    **NAMBA YAKO YA MTIHANI**
    **JINA LAKO**
    **JINA LA SHULE YAKO**

5. Kwa kuchora kistari katika visanduku vyenye namba zinazokuhusu, onyesha namba yako kamili ya mtihani (yaani namba ya shule, na zile namba tatu za mtahiniwa) katika sehemu iliyotengwa mwanzo wa karatasi ya majibu.
6. Usitie alama zozote nje ya visanduku.
7. Iweke safi karatasi yako ya majibu na usiikunje.
8. Kwa kila swali 1-50 umepewa majibu manne. Majibu hayo yameonyeshwa kwa herufi A, B, C, D. Ni jibu MOJA tu kati ya hayo manne ambalo ni sahihi. Chagua jibu hilo.
9. Kwenye karatasi ya majibu, jibu sahihi lionyeshwe kwa kuchora kistari katika kisanduku chenye herufi uliyochagua kuwa ndilo jibu.

    **Mfano:**

    **Katika kijitabu cha maswali:**

    **22.** Barua ya kuomba kazi huitwa
    A. waraka
    B. barua maalum
    C. barua ya kiofisi
    D. Barua rasmi

    Jibu sahihi ni **D**

    **Katika karatasi ya majibu:**

    **2.** [A] [B] [C] [D] **12.** [A] [B] [C] [D] **22.** [A] [B] [C] [D] **32.** [A] [B] [C] [D] **42.** [A] [B] [C] [D]

    Katika visanduku vinavyoonyesha majibu ya swali namba **22**, kisanduku chenye herufi **D** ndicho kilichochorwa kistari.

10. Chora kistari chako vizuri. Kistari chako kiwe cheusi na kisijitokeze nje ya kisanduku.
11. Kwa kila swali, chora kistari katika kisanduku **kimoja tu** kati ya visanduku vinne ulivyopewa.

**Kijitabu hiki cha maswali kina kurasa 7 zilizopigwa chapa.**

906504

© *Mtihani Bora*

**GEUZA UKURASA**

***Soma vifungu vifuatavyo. Vina nafasi 1 mpaka 15. Kwa kila nafasi umepewa majibu manne hapo. Chagua jibu lifaalo zaidi kati ya yale uliyopewa.***

Ni __1__ mtupu kuona baadhi ya jamii __2__ mtoto hususan msichana kama __3__ cha kunasia utajiri. Katika jamii husika __4__ kukiona kisichana kikiburutwa kutoka shuleni na __5__ kwa shaibu wa __6__ ya babuye. __7__ mwacha mila ni mtumwa, kamwe tusikubali kuwa watumwa wa baadhi za mila zilizopitwa na wakati.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 1. | A. uraibu | B. ustaarabu | C. ushenzi | D. kifaa |
| 2. | A. yakimchukulia | B. zikimchukulia | C. kimchukulia | D. likimchukua |
| 3. | A. chambo | B. chombo | C. mtego | D. kifaa |
| 4. | A. si nadra | B. ni nadra | C. vigumu | D. si rahisi |
| 5. | A. kuoelewa | B. kuoa | C. kuozeshwa | D. kuozwa |
| 6. | A. hirimu | B. nasaba | C. rafiki | D. somo |
| 7. | A. Isipokuwa | B. Ijapokuwa | C. Hata | D. Licha ya |

Nilipokuwa nikizungukazunguka huko na huko __8__, nilimsikia __9__ mmoja mwenye __10__ ya mguu akisema kwa kukejeli: "Hakuna __11__ siku hizi, hata ndugu __12__ kumkopesha __13__ kwani kukopa arusi kulipa __14__ " Kwa __15__, maneno yake yalinichoma moyo.

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 8. | A. mataani | B. manyumbani | C. mabarabarani | D. mitaani |
| 9. | A. kilema | B. kasoro | C. kombo | D. kiatu |
| 10. | A. kasoro | B. kombo | C. kilema | D. kiatu |
| 11. | A. amani | B. amana | C. amini | D. imani |
| 12. | A. hakubali | B. haitikii | C. hasemi | D. hakatai |
| 13. | A. nduguke | B. nduguyo | C. nduguye | D. ndugue |
| 14. | A. matanga | B. talaka | C. msiba | D. matata |
| 15. | A. makini | B. yakini | C. yamkini | D. lakini |

***Kutoka swali la 16 mpaka 30, chagua jibu lililo sahihi.***

16. Chagua kiwakilishi na kielezi katika sentensi ifuatayo
Huyu jongoo ananyiririka polepole.
A. huyu, ananyiririka
B. ananyiririka, polepole
C. jongoo, polepole
D. huyu, polepole

17. Mchwa ni kwa kichuguu kama vile wavulana waliotiwa jando ni kwa:-
A. kifukofuko
B. unyagoni
C. kumbi
D. kitala

18. Sentensi adhibiwa kijeshi ni:-
A. tashbihi
B. takriri
C. istiara
D. nahau

19. Maana ya semi 'pandwa na mori' ni
A. patwa na huzuni
B. hatwa na hasira
C. kosa kukufunikiwa
D. pata maafa

20. Basi lilikuwa na abiria kumi na wawili ________ dereva na utingo.
A. mithili ya
B. licha ya
C. mighairi ya
D. fauka ya

21. Jibu la maamkizi karibu tule ni:-
A. chewa
B. inshallah
C. majaliwa
D. starehe

22. Kutoa talaka ni:-
A. kufunga ndoa
B. kuvunja ndoa
C. kufunja ndoa
D. kuoana

23. ***Chagua usemi halisi wa:***
Mama aliwauliza kama wangeenda sokoni siku hiyo jioni.
A. "Mtaenda sokoni leo jioni?" Mama aliwauliza
B. "Mtaenda sokoni kesho jioni?" Mama aliwauliza
C. "Kesho jioni mngeenda sokoni?" Mama aliwauliza.
D. "Leo jioni mngeenda sokoni?" Mama aliwauliza.

24. Chagua sehemu za ndani za mwili.
A. Buki, ufizi, nyonga, pafu
B. Bandama, wengu, chango, umio
C. Muundi, kisogo paji, shahada
D. Figo, uso, mshipa, kisukusuku

25. ***Ukubwa wa sentensi.***
*'Ng'ombe wenye ndama waliwashambulia ndovu wengi'* ni
A. magombe yenye madama yaliyashambulia madovu mengi
B. majigombe wenye majidama waliwashambulia majidovu mengi
C. magombe wenye madama waliwashambulia madovu wengi
D. mang'ombe yenye mandama yaliwashambulia mandovu mengi

26. Sinia kubwa ya ubao ya kupakulia chakula ni huitwa:-
A. susu
B. buli
C. chano
D. kinu

27. Ndugu mdogo huitwa:-
A. mlamu
B. mcheja
C. umbu
D. mnuna

28. ***Kanusha sentensi ifuatayo.***
Tungalimwona tungalimsaidia
A. Tusingalimwona tusingalimsaidia
B. Tusingemwona tusingemsaidia
C. Tusingalimwona tungemsaidia
D. Tusingemwona tusingalimsaidia

29. Mchezo wa kuvutana kwa kamba ni:-
A. langalanga
B. jugwe
C. mlenge
D. kwata

30. Chagua jozi ya visawe.
A. njia - baraste
B. bandika - bandua
C. bawabu - bawaba
D. panda - panda

**_Soma taarifa hii kisha ujibu maswali 31-40._**

Bwana Kopa alidaiwa kope si zake. Alikuwa na madeni mzomzo kutoka majaribu mbalimbali. Alidaiwa na marafiki zake, wafanyakazi wenzake, mwajiri wake na majirani zake. Dukani nako alikuwa kakopa bidhaa na kushindwa kulipa.

Hulka hii ya kukopa ilimwanza angali mdogo shuleni alipoanza kuombaomba vitu kama kalamu, raba na rula. Ikaendelea alipokua na kuota mizizi alipoanza kukopa pesa kutoka kila mahali palipowezekana.

Naam, kukopa harusi kulipa matanga. Bwana Kopa aliona rahisi kukopa lakini kulipa aliona vigumu. Kamwe hakulipa deni alipokopa. Wenzake walimtahadharisha ajiepushe na kukopa ovyo ovyo lakini katu hakusikia la mwadhini wala la mteka maji msikitini.

Alipoajiriwa, alitumia ile fursa kuchukua bidhaa za mkopo kwa wakopeshaji bidhaa kwa malipo ya polepole. Mshahara wake ukawa unakatwa hata kabla haujamfikia. Mshahara ulipokosa kutosha, alichukua mkopo kutoka kwa shirika lao pale kazini. Pesa alizokopa alizitumia shaghalabaghala bila ya kuziekeza katika miradi ambayo ingemletea faida.

Wakati mwingine, alipodaiwa na mtu mmoja alienda kukopa kwa wa pili ili kumlipa wa kwanza. Hali hii ilimfanya Kopa azame zaidi katika lindi la matatizo. Kila aendapo, watu wakawa wanamhepa kwa kuhofu atawakopa. Wengine wakawa daima wanamtafuta kwa udi na uvumba kudai malipo yao.

Maji yalipozidi unga, akaanza kuuza bidhaa za nyumba kujaribu kupata ghawazi. Wakati huo huo bidhaa nyingine zikatwaliwa na waliomkopesha ili wafidie hasara zao. Uhawinde ukaanza kubisha hodi kwa Kopa.

Ilitokea siku moja Kopa akapata kusikia habari za bibi mmoja ambaye hukopesha pesa kwa riba ambayo Kopa aliiona nafuu. Mara akasahau kuwa vioevu si maji. Akakimbilia wazo lile. Alishika tariki hadi kwa yule bibi. Wakakutana. Baada ya mazungumzo marefu waliafikiana mkataba fulani na Kopa akapewa mkopo aliohitaji. Alirudi kwake akiwa amejawa na bashashi ghaya iliyodhihirishwa na tabasamu aliyokuwa nayo mdomoni.

Njenje alizopata hakuzitumia kwa njia ambayo ingemletea tija ili aweze kuzilipa. Mkataba wa malipo kwa bibi aliyemkopesha ulikuwa kwamba baada ya kipindi cha mwezi mmoja angeanza kulipa polepole kila mwezi. Safari ya kwanza alilipa kama walivyoahidiana. Mwezi wa pili akalipa akiwa amechelewa. Mwezi wa tatu hakulipa. Wa nne ukapita bila kutimiza ahadi. Miezi ikawa mwaka bila kulipa deni lile. Ndiposa yule bibi alipokosa subira tena na kumpeleka Kopa kwa wakili. Kopa akafunguliwa mashtaka kortini na akashindwa kujitetea. Mdai wake alimlipia sima gerezani ambapo mdaiwa hubidiika kufungwa hadi atakapolipa deni.

Ama kwa kweli, asiyefunzwa na mamaye hufunzwa na ulimwengu.

---

**31.** Ni nahau gani inayoonyesha kuwa Bwana Kopa alikuwa na madeni mengi?
A. Maneno mbalimbali  B. Daiwa kope si zake
C. Alidaiwa  D. Kutolipa

**32.** Yaelekea Bwana Kopa alianza Kuomba
A. kutokana na shida  B. alipokuwa mdogo
C. kitabia tu  D. iliaweze kusoma

**33.** Maana ya ***'kuota mizizi'*** kama ilivyotumika hapa ni kuwa tabia:-
A. ikamea  B. ikazidi
C. ikasamba  D. ikakolea

**34.** Kwa nini wenzake Kopa walimwonya ?
A. Kukopa harusi kulipa matanga
B. Alikopa ovyo ovyo
C. Aliona vigumu kulipa
D. Alikataa kulipa deni

**35.** Kwa nini mshahara wa Kopa ulikatwa?
A. Alikosa kulipa deni
B. Alikuwa na madeni mengi kazini
C. Kulipa bidhaa kwa wakopeshaji
D. Hakuwa anafanya kazi isipokuwa kukopa

**36.** Watu waliomtafuta Kopa walikuwa:-
A. wadai wake
B. wadeni wake
C. wadaiwa wake
D. wa udi na uvumba

**37.** Maana ya **'wafidie'** ni:-
A. waondoe  B. wafikie
C. wafaidike  D. walipie hasara

**38.** Riba ni
A. faida ya pesa zilizokopeshwa
B. mkopo wa pesa
C. mkataba wa kukopesha
D. malipo ya mkopo

**39.** Tunaweza kusema Bwana Kopa alikuwa
A. mtiifu  B. mbadhirifu
C. mfitini  D. mwaminifu

**40.** Hatima ya Kopa ilikuwa ni
A. kushtakiwa
B. kuhukumiwa
C. kufungwa
D. kortini

***Soma taarifa hii kisha ujibu maswali 41-50.***

Aghalabu, barobaro hupenda mambo makubwa zaidi ya yale waliyo nayo. Hupenda kutofungwa na sheria yoyote ili wapate kufanya mambo jinsi wapendavyo. Lakini hivi sivyo. Mwana hana budi kutii kanuni za kiamboni; mtoto lazima amkabili abu na nina kwa adabu. Lazima afundishwe utu na kuutambua. Na chini ya maelekezo kama haya, mtoto hawezi kusema ati amenyimwa uhuru! Sharti itambulike kuwa darasa la kwanza la mtoto ni nyumbani, la pili ni shuleni na la tatu katika maisha. Mvyele mwema hupenda kumwona mtoto wake akikua kwa adabu ili kuimarisha jina lake.

Katika uwanja huu wa utamaduni wanachuoni wanaangaliwa sana kwamba watautetea utamaduni wao kama vile wazee wao walivyosimama kidete. Wanachuoni mkisinzia, fedheha itakuwa kwenu! Sisi wazee, tulijiendea tu pasipo taa. Lakini nyinyi vijana mna taa. Kwa msaada wa taa hizo, nyinyi ndio mpasao kuutunza utamaduni huo. Je ni nani atasimama kadamnasi na kumkataa baba yake kuwa si baba? Tambua kuwa yeye ni chaza katoa lulu. Utamaduni wetu ndiye baba yetu.

Tabia za kigeni ni tofauti sana na zetu. Kwa mfano, mtindo wa kuamkiana, kula pamoja, mdogo kumjua mkubwa, mkubwa kumjua mdogo na kadhalika katika kuamkiana. Sisi waafrika hatuna hulka ya kupitana njiani kimya kimya tu. Ni kawaida yetu kuamkiana njiani na kujuliana hali. Kwa njia hii, watu huweza kujuana hata kwa undani zaidi.

Adinasi wana namna za miiko. Binadamu ni mnyama razini wala si hayawani. Wenye dini na wasio na dini hukutana kumlinda mwanadamu na haki zake za ubinadamu.

**41.** Kulingana na ufahamu, kwa nini vijana wa siku hizi hawataki kufuata mila na desturi za asili?
A. Wamesoma sana
B. Wana elimu
C. Wameathiriwa na mwigo na mambo ya kigeni
D. Hawana adabu wala hawatii wazazi wao

**42.** Kutotii kanuni za nyumbani kunasababisha:-
A. kutofungwa na sheria yoyote
B. watoto waishi wapendavyo
C. chuki kati ya wazee na vijana
D. watoto wakose adabu

**43.** Mwana hujifunza utu na adabu kutokana na:-
A. wazazi, mila na jamii
B. marafiki na watoto wenziwe
C. elimu yake chuoni
D. kumkabili baba na mama

**44.** Kwa mujibu wa habari hii, elimu ya mtoto huanzia:-
A. kwa mwalimu
B. kwa wazazi
C. shuleni
D. katika darasa la kwanza

**45.** Wanachuoni wanaangaliwa sana kwamba watautetea utamaduni kwa kutumia:-
A. elimu waliyo nayo
B. taa walizo nazo
C. chuo chao
D. msaada wa wazee wao

**46.** Mwandishi amemthilisha utamaduni na:-
A. taa　　B. baba
C. cheza　　D. lulu

**47.** Ni ipi si tofauti kati ya desturi za kiafrika na za kigeni?
A. Kusalimiana
B. Kupishana njia kimyakimya
C. Kutokula pamoja
D. Mdogo na mkubwa kujuana

**48.** Binadamu ni mnyama **razini.** Maana yake ni kuwa:-
A. ana uwezo wa kujuana na wenzake
B. ana adabu
C. anaweza kutembea miguu miwili si kama hayawani
D. ana uwezo wa kufikiri

**49.** Dhamira kuu ya habari hii ni:-
A. kuwakanya watoto wasiufuate utamaduni wa kigeni
B. kutoa wito kwa vijana waliosoma wautetee utamaduni wetu
C. kuwahimiza wazazi na wasomi wawafunze watoto wetu kufuata utamaduni ili wasipotoke maishani
D. kuelezea kuwa utamaduni wa kigeni ni tofauti na wa kiafrika

**50.** Methali bora kwa habari hii ni:-
A. Asiyesikia la mkuu huvunjika guu
B. Mwacha mila ni mtumwa
C. Mkaidi hafaidi hadi siku ya Idd
D. Mtoto wa nyoka ni nyoka

**Andika insha ya kusisimua itakayomalizikia kwa maneno yafuatayo:**

.................. *wote waliniangalia kwa furaha na kunipigia makofi ya heko*